



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA
MADINI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA KUENZIA JANUARI, 2016
HADI JANUARI, 2017**

***[Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]***

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
Dodoma

7 FEBRUARI, 2017

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA
MADINI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA KUENZIAJANUARI, 2016
HADI JANUARI, 2017**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ni moja ya Kamati ya kisekta yenye majukumu mbalimbali yaliyoanishwa kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Nishati na Madini inawajibu wa kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka kuhusu utekelezaji wa majukumu yake katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, sitoweza kusoma taarifa yote. Hivyo naomba taarifa yote, pamoja na sehemu ambazo sitozisoma ichukuliwe kwenye Hansard.

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2016, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanunikama ilivyoanishwa katika Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Pamoja na majukumu mengine Kamati imetekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini
- b) Kushughulikia Taarifa za Mwaka za Utendaji wa Wizara ya Nishati na Madini pamoja na;
- c) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo.

1.2 Njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yakekama yalivyoanishwa kwenye Kanuni hapo juu, Kamati ilitumia njia mbalimbali ili kufanikisha majukumu yake. Ukaguzi wa miradi, kupokea taarifa mbalimbali, majadiliano na Wizara pamoja na taasisi zake, mafunzo na semina zilifanikisha Kamati kufikia malengo yake ya utekelezaji wa majukumu yake ya Kikanuni.

1.2.1 Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitokeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara ya Nishati na Madini.

Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Manyara, Njombe na Mbeya kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati na Madini iliyotengewa fedha na kupelekewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyokaguliwana Kamati yako kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama ifuatavyo;

- i) Mradi wa Kuzalisha umeme wa Kinyerezi I MW 150,
- ii) Mradi wa Bomba la Gesi Mtwara,
- iii) Mradi wa Makambako/Songea Transmission line 220kv na
- iv) Miradi ya umeme vijijini (REA) katika mkoa wa Njombe.
- v) Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira
- vi) Mgodini wa Tanzanite One

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi uliofanywa na Kamati yako, zilibainika changamoto mbalimbali zinazochangia kuzorota kwa utekelezaji wa Miradi katika maeneo mbalimbali hasa yaliyokaguliwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Wizara ya Nishati na Madini kutengewa Bajeti ya kutosha kila mwaka kwenye miradi ya maendeleo, Kamati imekuwa ikisikitishwa na upelekaji hafifu wa fedha hizo, hasa kwenye miradi ya REA ambayo fedha zake ni rahisi kukusanywa na zina wigo wa Kisheria yaani (*Ring fenced*).

Mheshimiwa Spika, Toka kuanza kwa Mfuko wa Umeme vijijini mwaka 2013 hadi Disemba, 2016 Mfuko ulipaswa kuwa umepokea jumla ya shilingi Bilioni 749 ambazo ni makusanyo ya tozo za Mafuta yaliyoingia nchini katika kipindi hicho pamoja na makusanyo yatokanayo na *Customs processing Fee*.

Aidha, katika kipindi hicho cha kuanzia mwaka 2013 hadi Disemba, 2016 Mfuko wa REA umepokea jumla ya Shilingi Bilioni 630. 99 na Bakaa ya jumla ya Shilingi Bilioni 105.67 hazijawapelekwa katika Mfuko hadi sasa, Hali hii inasababisha kurudisha nyuma kasi ya utekelezaji wa Miradi.

Mheshimiwa Spika, kitendo hiki cha Serikali kutopeleka fedha za REA zinazotokana natozo mbalimbali za Mafuta kwa Wananchi kinaleta hisia mbaya kwa Kamati na Bunge lako kwa jumla kuwa Serikali inashindwa kuheshimu utaratibu uliowekwa kisheria wa kuzilinda fedha hizi.


Mheshimiwa Spika, Upelekeaji wa fedha za Miradi ya REA usiyoridhisha kumesababisha miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati. Pia kuchelewesha malipo kwa wakandarasi kuna sababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hiyo kwa mwaka husika. Kielelezo namba moja na namba mbili kinatoa ufafanuzi kuhusu mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka husika pamoja na ufafanuzi wa upatikanaji huo kwa asilimia.

Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika kipindi cha miaka mitanokuanzia 2012/2013 hadi 2016/2017

Kielelezo: 1

MWAKA	KILICHODHINISHWA	KILICHOTOLEWA	%
2012/2013	531.2	-	0
2013/2014	1,100	614	55.81818
2014/2015	957.2	271.57	28.37129
2015/2016	502.3	579	115.2698
2016/2017	1060	291.30	25.95

MCHANGANUO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ZILIZODHINISHWA NA KUPOKELEWA NA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2012/2013 HADI 2016/2017.



Mheshimiwa Spika, Katika miradi mingi iliyokaguliwa na Kamati yako, Kamati ilikutana na changamoto kubwa ya usimamizi mbovu na usiyo ridhisha hasa katika miradi ya REA nakupelekea miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango katika maeneo mengi. Mfano miradi mingi ya REA katika mkoa wa njombe.

Aidha, mradi mingi ya sekta ya Madini iliyokaguliwa na Kamati yako ilikuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha za kuendeleza miradi hiyo kama vile Mgodini wa Makaa ya Mawe kiwira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na usimamizi mdogo na usiyoridhisha katika Mgodini wa Tanzanite One, mgodi ambao umekuwa hauna tija iliyokusudiwa na Taifa kupitia madini haya adhimu yanayopatikana Tanzania peke yake. Miongoni mwa mambo yanayochangia usimamizi usiyoridhisha ni pamoja na Migogoro ya muda mrefu ya wachimbaji wadogo wadogo na Mwekezaji wa Tanzanite One, Utoroshwaji wa Madini ya Tanzanite nje ya nchi pamoja na usimamizi mbovu wa Mgodini huo.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwenye Mgodini wa Tanzanite One kama vile ukaguzi maalumu na kuanzishwa kwa Mnada wa madini ya Vito, Kamati imebaini kuwa Madini haya yaliyouzwa kwenye mnada huo na kusafirishwa nje ya nchi yalikuwa ni ghafi kinyume na matakwa Sheria ya Madini 2010 pamoja nauamuzi wa Serikali wa kutokusafirisha madini hayo yakiwa ghafi.

Hivyo Kamati yako inaitaka Wizara kuhakikisha Sheria na kanuni zinazingatiwa katika uendeshaji wa Minada hiyo.

❖ **Ziara ya Kamati katika Migodini ya Buzwagi na Stamigold/ Tulawaka katika kipindi cha Januari, 2017**

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Januari, 2017 Kamati iliweza kutembelea Mgodini wa Stamigold kwa nia ya kujionea uendeshaji wa Mgodini huo unaomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Katika ziara hiyo Kamati imebaini changamoto kubwa zinazokwamisha utendaji na uzalishaji katika mgodini huo kama vile;

- a) Mgodini kukosafedha ya Mtaji wa kuendesha shughuli za Mgodini;

- b) Ukosefu wa Mitambo ya kufanyia kazi na hivyo kulazimika kukodisha kwa gharama ya juu;
- c) Kukosekana kwa misamaha ya kodi kwenye vifaa hasa mafuta yanayotumika kuendeshea shughuli za mgodi huo;
- d) Mgodi kutokuwa na Mining Development Agreement MDA kama Migodi mingi hapa nchini;
- e) Mgodi kushindwa kukopesheka kwa sababu ya kukosa umiliki halali wa Mali (Assets) za Mgodi; na
- f) Sheria ya Manunuzi inakwamisha ununuzi wa vipuri kwa haraka kwa ajili ya matengenezo.

Aidha, kamati inaitaka Wizara kuhakikisha changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi wa haraka ili kusaidia mgodi huo kuweza kujiendesha vizuri na kutengeneza faida inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ni matumaini ya Kamati kuwa, kwa mashapo yaliyopo katika Mgodi huo ukisimamiwa vizuri na Serikali itaongeza mapato ya nchi pamoja na sifa kwa nchi yetu kwa kuweza kuendesha mgodi wetu wenyewe bila kutegemea Wawekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Pia Kamati ilitembelea mgodi wa Buzwagi unaomilikiwa na kampuni ya ACACIA kwa lengo la kujionea utekelezaji na usimamizi wa sheria na kanuni katika Mpango wa maandalizi ya Kufunga Mgodi inavyotekelezwa katika Mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, Mgod huo unatarajia ifikapo Disemba, 2017 itafunga shughuli za uchimbaji kutokana na kiwango kidogo cha upatikanaji wa dhahabu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Mgod katika maandalizi hayo ya ufungaji wa shughuli zake, Kamati haikuridhishwa na maandalizi hayo kwa kuwa hayakubainisha ni lini hasa Mgod huo utakamilisha taratibu mbalimbali zinazotakiwa kufuatwa ili kuhitimisha shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya kamati kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, itahakikisha kuwa Mgod huu unakamilisha taratibu zote za Kisheria na za kikanuni, kama vile kulipa kodi mbalimbali za Serikali pamoja na za Halmashauri husika ili kuepuka usumbufu kama uliojitokeza katika Mgod wa Resolute ulipofunga shughuli zake za uchimbaji huko Nzega mkoani Tabora.

1.3.1 Ziara za mafunzo

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kusafiri kwenda nchini Bangladesh kwa ajili ya kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu sekta za Nishati Jadidifu (Renewable Energy). Lengo la ziara hii ilikuwa ni kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika masuala ya uzalishaji umeme unaotokana na vyanzo vingine ambavyo ni rahisi na vinapatikana katika mazingira yetu.

Mafunzo hayo yamekuza uelewa kwa Wajumbe kuhusu masuala ya Nishati Jadidifu na hivyo kuwasaidia kutoa ushauri kwa Wizara ya Nishati na Madini kuhusu uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo vingine kama upepo, jua pamoja na Tungamo Taka.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo Wajumbe walipata wasaa wa kukutana na viongozi mbalimbali wa Serikali kama Mshauri wa Waziri Mkuu katika masuala ya

Nishati, ambaye aliwaeleza wajumbe kuwa kutokana na kuendelea kuharibika kwa mazingira, Bangladesh imejipanga kuhakikisha inatumia vyanzo vya nishati ya umeme ambavyo ni rafiki kwa mazingira kama vile kuzalisha jua, tungamotaka na upepo.

1.3.2 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kuendelea kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati yako, Ofisi ya Bunge iliandaa mafunzo ya siku moja kupitia mradi wa *UNDP (Legislative Support Program)* kuhusu masuala ya kutunga Sheria pamoja na Kanuni mbalimbali.

Pia Wizara ya Nishati na Madini iliomba kuwapatia wajumbe wa Kamati Semina ya siku moja kuhusu Miradi kabambe itakayotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

Lengo la mafunzo haya ya Wizara lilikuwa nikuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati kuifahamu vyema miradi Kabambe pamoja na ile ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi isiyo ya kiserikali ya *Natural Resource Government Institute (NRGI)* imekuwa msaada sana kwa Kamati hii kwa kuandaa Seminambalimbali za kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika sekta hizi muhimu za madini, mafuta na gesi.

Semina hizo zimekuwa zikilenga kuwajengea uwezo wajumbe kuhusu Sheria mbalimbali zinazohusu udhibiti na ukusanyaji wa Mapato kutoka kwenye Sekta hizi kwa maendeleo ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kupitia mafunzo haya Kamati yako ya Nishati na Madini imekuwa na uelewa wa kuhusu sekta hizi muhimu inazosisimamia kwa kuelewa

vyema mambo muhimu ya kuzingatia kama Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kushauri na kuisimamia Wizara ya Nishati na Madini.

2.0 KAZI MAHSUSI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Nishati na Madinikatika kipindi cha mwaka mzimaimetekeleza majukumu yafuatavyo:-

- i) Kupokea Taarifa ya nusu Mwaka ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016;
- ii) Kupokea na kujadili taarifa za utendaji wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini
- iii) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016; na
- iv) Kupokea na Kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 pamoja na uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

2.1 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Ujumla

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kurejea hati idhini ya Serikali namba 144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 (Government instrument). Lengo lilikuwa ni kuoanisha bajeti inayotengwa, iliyopokelewa, matokeo ya utekelezaji wa bajeti na matarajio ya wananchi kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa Bajeti kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha nusu mwaka (kuanzia Julai hadi Disemba 2016) na kubaini kuwa hadi kufikiatarehe 31 Desemba, 2016 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya bilioni 291.30, sawa na asilimia 25.95 ya Bajeti yote iliyotengwa na kuidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mheshimiwa Spika, Shilingi bilioni 267.53 sawa na asilimia 36.90 ni fedha za miradi ya maendeleo na Shilingi Bilioni 11.0 sawa na asilimia 28.30 ni fedha za matumizi mengineyo. Tafsiri ya upatikanaji wa fedha kwa kiwango hiki unatishia utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi husika .

SEHEMU YA PILI

3.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI YA NISHATI NA MADINI

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utendaji wa Wizara, Kamati iliweza kupokea taarifa mbalimbali zinazohusu sekta ya Nishati, Madini pamoja na sekta ndogo ya Mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, Katika kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa sekta ndogo ya mafuta pamoja na kupokea taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, taasisi zifuatazo zilizowasilisha taarifa kwenye Kamati na kujadiliwa.

3.1 Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wakala wa Umeme vijijini kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme kwa awamu ya pili na uanzishwaji wa mradi wa awamu ya tatu na kubaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa Wakala huu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Ucheleweshwaji na upelekaji wa fedha usioridhisha kwenye miradi ya REA umekuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa miradi hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu pamoja na fedha hizo kuwa nawigo wa kisheria;

- b) Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa Miradi kwa kushindwa kulipa Wakandarasi kwa wakati;
- c) Usimamizi usiyoridhisha kwa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi hiyo katika maeneo mbalimbali nchini; na
- d) Ushirikishwaji mdogo wa Viongozi katika maeneo ya miradi hasa wakati wa uainishaji wa vijiji/vitongoji umesababisha vijiji vingi kurukwa katika zoezi hili la uunganishaji wa umeme.

3.2 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Shirika la umeme TANESCO lenye jukumu la kuzalisha /kufua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

- a) Shirika linadaiwa jumla ya Shilingi Bilioni 822, deni hili linasababisha kuzorota kwa utendaji wa Shirika;
- b) Wateja wengi zikiwemo Wizara na Taasisi nyingi za Serikali kutolipa ankara zao kwa wakati. Kwa mfano Serikali peke yake, inadaiwa na TANESCO zaidi ya shilingi bilioni 269 ambazo imekuwa ikilipa kidogo kidogo na hivyo kukwamisha shughuli za TANESCO kutekelezeka kwa wakati;
- c) Uharibifu wa Mitambo ya kufua umeme inayopelekea mitambo hiyo kuzimwa kwa muda mrefu, kuna ligharimu shirika na Taifa kwa ujumla kwa kukosekana kwa umeme wa uhakikakatika maeneo mengi hapa nchini;
- d) Ukosefu wa umeme wa kutosha kunakotokana na Serikali kushindwa kuwekeza kwenye mitambo ya kuzalisha umeme kwa muda mrefu licha ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini; na

- e) Uchakavu wa miundombinu unaosababisha umeme mwingi kupotea njiani na hivyo kupunguza kiwango cha umeme kinachowafikia wananchi.

3.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini. Pamoja na mafanikio yaliyopo hasa kutokana na kugundulika kwa gesi nchini bado manufaa yake kwa wananchi hayajaonekana kwa kiasi cha kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha nusu mwaka hakuna fedha yeyote ya miradi ya maendeleo iliyotolewa na Serikali. Hivyo, miradi na tafiti nyingi zilizopangwa kufanyika katika kipindi hiki cha nusu mwaka hazijaweza kutekelezeka. Kamati inasikitishwa na hali hiyo kwa kuwa nia ya Shirika/ Kampuni hii kujiendasha kibiashara itashindikana.

Aidha, shirika linawadai wateja wake wakubwa jumla ya shilingi bilioni 307.47 kutolipwa kwa fedha hizi kwa wakati na kulifanya shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na shirika hili katika ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vingine, bado linakabiliwa na changamoto zifuatazo;

- a) Ukosefu wa soko la uhakika na lakuaminika la gesi inayozalishwa nchini;
- b) Bajeti ndogo inayotengwa kwa Shirika inapelekea shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake muhimu kwa Taifa hasa ya uwekezaji na utafiti wa gesi na mafuta nchini;

- c) Serikali kutokupeleka fedha za miradi kwa wakati kunasababisha miradi hiyokutokutekelezeka. Kwa mfano mradi wa kusambaza Gesi katika mkoa wa Dar Es Salaam.

3.4 Chuo cha Madini Dodoma

Sikazi wa Chuo cha Madini Dodoma ambacho kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundi sanifu, ushauri na utafiti katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kimeendelea kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2016 Chuo kilikuwa kimepokea jumla ya Shilingi Milioni 324.4 sawa ma asilimia 24.6 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2016/17. Utolewaji huu wa fedha hauridhishi kwani unakwamisha maendeleo ya chuo hiki muhimu kinachotusaidia Taifa kupata Mafundi sanifu na Mafundi Mchundo ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta hii ya Madini.

Pamoja na mafanikio mbalimbali ambayo Kamati ilielezwa, changamoto kubwa zifuatazo zilibainika:-

- a) Bajeti ndogo inayotengewa inakwamisha utekelezaji wa majukumu;
- b) Idadi ndogo ya madarasa ya kufundishia;
- c) Uhaba wa wakufunzi hasa katika fani za jiolojia, uhandisi migodi, fizikia na kompyuta; na
- d) Hakuna sehemu za kutosha za wanafunzi wao kufanyia mafunzo kwa vitendo.

3.5 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa majukumu yanayotekelezwa na Wakala wa Jiolojia ambayo ni kukusanya, kuchambua, kutafsiri, kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za kijiosayansi (jiolojia, Jiokemia na jiofizikia), kutengeneza na kusambaza ramani, takwimu na taarifa mbalimbali zinazoainisha kuwepo kwa aina mbalimba za miamba nchini.

Mheshimiwa Spika, Wakala hufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti

mbalimali nchini na kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi, mionzi asili n.k.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu hayamazito waliyonayo GST changamoto zifuatazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa majukumu yake:-

- a) Bajeti inayotengewa ni ndogo na haitolewi yote hususan ya miradi ya maendeleo, hivyo kushindwa kutekeleza Miradi kwa wakati;
- b) Uhaba wa Vifaa maalum vya kisayansi vya kufanyia kazi; na
- c) Ukosefu wa watumishi wa kutosha.

3.6 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Stamico. Shirika hili la madini limepewa jukumu la kusimamia sekta ya madini kwa kufanya tafiti na uwekezaji katika migodi ya madini kama zilivyo kampuni zingine kwaniaba ya serikali.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili lilitengewa na kuidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya Shilingi Bilioni 6.8, hadi kufikia Disemba, 2016 shirika lilipokea jumla ya shilingi Bilioni 1.34 sawa na asilimia 20 ya Bajeti iliyoidhinishwa, ambapo mishahara ni asilimia 16 na matumizi mengineyo ni asilimia 4 ya bajeti hiyo, Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, Shirika limekwama kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu ya msingi ya kuendeleza Sekta ya Madini kutokana na changamoto zifuatavyo:-

- a) Ukosefu wa Fedha unaosababisha kukwama kwa shughuli nyingi za shirika hilo. Aidha, ukosefu wa mtaji wa kuanzisha/ kuwekeza katika miradi mingine,
- b) Miradi mingi waliyowekeza hadi sasa hawajaanza kupata faida, kwa mfano Mgodi wa Tanzanite one, Stamigold/Tulawaka, Kiwira n.k;

- c) Pia shirika limekabidhiwa majukumu mengi pamoja na bajeti ndogo wanayopewa kwa mwaka.
- d) Ukosefu wa Mikataba katika migodi ya Stamigold na Kiwira kuna pelekea migodi hii kushindwa kukopesheka.

4.0 Sekta Ndogo ya Mafuta na hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Wizara pamoja na wadau wa Sekta ndogo ya mafuta nchini kuhusu mfumo mzima wa uingizaji wa mafuta pamoja na maendeleo ya sekta hiyo. Katika taarifa hizo Kamati ilipata uelewa wa hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya Serikali ya kuanzisha Wakala wa uingizaji wa mafuta kwa Pamoja nchini, Sekta hii bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

- a) Ukosefu wa Matanki makubwa ya kuhifadhi mafuta (*Farm Tanks*) baada ya kupakuliwa kutoka Melinikunasababisha hasara kwa Makampuni yanayoingiza mafuta pamoja na kuikosesha Serikali mapato;
- b) Usalama mdogo wa mabomba yanayotumika kupakulia na kusambazia mafuta hasa ya KOJ-1, na hivyo kusababisha Makampuni yanayoagiza mafuta yatumie gharama kubwa kwa ajili ya ulinzi;
- c) Gharama kubwa ya uwekaji wa Vinasaba (Tsh. 12 kwa lita) ikilinganishwa na nchi jirani kama Kenya gharama ni Tsh. 1 kwa lita na Uganda Tsh. 2 kuna muongozea mzigo mwananchi.
- d) Tozo za Taasisi mbalimbali za Serikali kwenye bei ya Mafuta ni mzigokwa Wafanyabiashara wa Sekta ya mafuta;
- e) Bei elekezi ya Mafuta haizingatii maeneo yaliyo mbali na Miji/Makao Makuu ya Wilaya na hivyo kusababisha wananchi waliopo katika maeneo hayo kupata nishati hii kwa bei ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, Ukosefu wa Matanki ya kuhifadhia Mafuta yaani (*Farm Tanks*) ni changamoto kubwa ambayo Serikali inatakiwa kuchukua hatua za madhubuti ili kuokoa mapato ya Serikali yanayopotea kila siku kutoka katika Sekta hii. Aidha, kwa kuwa TPDC ina maeneo ambayo mradi huu unaweza kutekelezwa, ni vyema Serikali ikaiwezesha TPDC kupitia Kampuni tanzu ya COPEC kuwekeza katika ujenzi wa Matanki hayo.

4.1 Sekta ya Madini

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa sekta hii imekuwa ikilalamikiwa sana na Wananchi wengi hasa wanaoishi maeneo ya migodi kuwa ni sekta ambayo haitoi mchango mkubwa katika pato la Taifa kama ilivyo katika nchi nyingine zenye Rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, Na kwa kuwa, Madini ni Rasilimali inayokwisha ni vyema Serikali ikaweka mkazo katika kusimamia sekta hii kwa kuziwezesha Taasisi zinazosimamia upatikanaji na udhibiti wa mapato yanatokanayo na madini kwa kuzitengea bajeti ya kutosha na kuzipelekea fedha hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Utoaji ruzuku kwa wachimbaji wadogo ni jambo zuri sana katika kuisaidia Sekta hii, hasa kuwasaidia na kuwaendeleza wachimbaji wadogo hapa nchini. Aidha, ni hofu ya Kamati kuwa fedha hizi za ruzuku zisiposimamiwa vyema hazitaweza kuleta tija na kukidhi lengo la kuwasaidia wachimbaji wadogo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe kuwa Wachimbaji wadogo wadogo pamoja na Wananchi waliopisha Wawekezaji wanalipwa fidia stahiki, na kutengewa maeneo mengine ya kuendeleza shughuli zao za uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za maksudi walizochukua ili kuokoa maisha ya Wachimbaji wadogo wadogo 15 waliokuwa wamefukiwa na kifusi katika Mgodi mdogo wa

Nyarugusu. Ni rai ya Kamti kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini waongeze jitihada ya kutoa Elimu kuhusu mbinu bora za uchimbaji wa Madini hasa kwa Wachimbaji wadogo wadogo katika nchi yetu. Aidha, elimu hii itasaidia kupunguza matukio ya aina hii kwa Wachimbaji wadogo wadogo.

4.2 Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini

Mheshimiwa Spika, Hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika katika maeneo mengi hususani vijijini, mafanikio haya yametokana na ukamilishwaji wa miradi mingi ya REA awamu ya kwanza na awamu ya pili.

Kwa sasa nchi yetu inawezwa kuzalisha MW 1300 na matumizi ya juu kabisa ya nchi yetu yameweza kufikia hadi MW 1041, matumizi haya yakadiriwa kuongezeka siku hadi siku kutokana mahitaji ya nishati hii kukua kwa kasi nchini.

Mheshimiwa Spika, mahitaji haya ya umeme yanapaswa kabisa kuendana na kasi ya ukamilishaji wa miradi mingi ya Umeme inayotekelezwa hapa nchini, Kamati inaishauri na kuitaka Serikali kupeleka fedha katika miradi yote ya umeme ili iweze kukamilika kwa wakati na kufikia malengo ya wizara iliyojiwekea ya kufika MW 5000 ifikapo 2021.

Mheshimiwa Spika, ili nchi yetu iweze kuwa nchi ya Viwanda ni lazima miradi mingi ya umeme ipelekewe fedha kama ilivyopangwa hasa kwa miradi ya REA inayotekelezwa nchi nzima. Aidha, ukarabati na matengenezo ya Mitambo ya kufua umeme ni jambo la muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

4.3 Kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na mchakato wa bajeti wa wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka Fedha 2015/2016 pamoja na kuchambua Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 miradi mingi ya umeme hasa ya REA imeshindwa kukamilika kwa wakati kwa sababu ya ukosefu wa fedha na usimamizi mbovu wa miradi hiyo iliyosabisha miradi mingi kutekelezwa chini ya kiwango katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya Kamati ilivyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 19 Mei, 2016 tunaipongeza Serikali kwa kutenga bajeti ya kutosha katika miradi ya maendeleo hususani miradi ya umeme itakayosaidia wananchi kupata umeme wa uhakika katika maeneo mengi ya nchi na kupelekea uchumi wa viwanda kutekelezeka kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Hivyo basi, ni ushauri wa kamati kuwa bajeti iliyotengwa ya miradi ya maendeleo itolewe yote na kwa wakati na kuwe na usimamizi mzuri wa fedha hizo ili ziweze kuleta tija.

Kamati inaendelea kusesitiza Serikali kufanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati kwa manufaa ya Taifa.

SEHEMU YA TATU

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

5.1 Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara ya Nishati na Madini, ziara za ukaguzi wa miradi pamoja na kukutana na Wadau wa sekta zote mbili za Nishati na Madini, Kamati ina maoni yafuatayo;

- a) Kutopatikana kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na Kamati kupitisha bajeti ya kutosha kila mwaka;
- b) Kukosekana kwa bei elekezi ya Mafuta kwenye maeneo yaliyo mbali na Miji/Makao Makuu ya Wilaya kunasababisha changamoto kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo;
- c) Kuwepo kwa tozo nyingi za taasisiza Serikali kwenye bei ya Mafuta ni kumuongezea mzigo mwananchi;
- d) Kutopatikana kwa fedha za miradi ya REA kwa wakati, kuna sababisha kuongezeka kwa gharama na muda wa ukamilishaji wa miradi hiyo;
- e) Upungufu wa Gati za kupakulia Mafuta kunasababisha msongamano wa Meli wakati wa kupakua mafuta, hivyo kufanya nchi jirani zishindwe kupitisha Mafuta katika Bandari zetu. Mfano; Meli moja inaweza kuchukua kati ya siku 4 – 8 kupakua mafuta;
- f) Ukosefuwa matanki ya kuhifadhia mafuta (Central Storage Facility) baada ya kupokea na kabla ya kusambaza kwenye depot za waagizaji wengine kunasababisha hasara kwa Serikali kwani inakosa takwimu sahihi za Mafuta yaliyoingia nchini;

- g) Utaratibu unaotumika wa kufunga *Flow Meters* kwenye meli badala ya kwenye Matanki ya kuhifadhia mafuta siyo sahihi kwa ajili ya kupata takwimu sahihi za mafuta yanayoingia nchini;
- h) Ukosefu wa fedha na bajeti ndogo inayotengwa na Serikali kwa taasisi ya TMAA, inaathiri utekelezaji wa majukumu muhimu ya taasisi hii;
- i) Serikali haina budi kuwaendeleza Wachimbaji wa Kati na Wadogo wadogo ili waweze kuendeleza sekta hii kwa uchumi wa Taifa letu;
- j) Ili kuwa na uwazi katika tasnia ya Uzinduaji ni vyema Serikali ikaiwezesha taasisi ya TEITI iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi;
- k) Serikali ifanye haraka kulipa Madeni ya Tanesco, ili kuipunguzia Shirika mzigo wa madeni hayo;
- l) Bunge liongezewe Bajeti ya kutosha ili kuliwezesha kutekeleza makujuku yake ya kikatiba, hasa ya kufanya ukaguzi katika miradi mingi inayotekelezwa na Serikali ili liweze kushauri ipasavyo.

5.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada kutekeleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, naomba kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

5.2.1 Wakala wa Nishati vijijini (REA)

a) Kutokupatikana kwa fedha za Miradi ya REA kwa wakati

Kwa kuwa, fedha za miradi ya REA zimekuwa zikichelewa kupelekwa na hupelekwa chini ya kiwango kilichokusanywa kutoka kwenye Tozo za Mafuta na hata zile zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu na kusababisha miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati;

Na kwa kuwa, kuchelewa kukamilika kwa miradi hupelekea Kuongezeka kwa gharama za Miradi husika kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo fidia kwa wakandarasi na kupanda kwa thamani ya dola hapa nchini;

Hivyo basi, Bunge lako liazimie kuwa fedha za miradi ya REA zipelekwe kwa wakati katika kutekeleza miradi hiyo kwa mwaka husika, ili kuipunguzia Serikali gharama ya kulipa fidia wakandarasi wanaocheleweshewa malipo yao.

b) Usimamizi wa Miradi ya REA

Kwa kuwa imebainika kuwa Miradi mingi ya REA iliyotekelezwa katika awamu ya kwanza na ya pili haikuwa na usimamizi mzuri,

Na kwa kuwa, usimamizi duni wa miradi hiyo ulisababisha kushindwa kutimiza malengo ya miradi ikiwemo kutokuwa na mashine humba (Transformer) zinazofanya kazi vizuri kwa muda mrefu,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri serikali kuhakikisha kuwa iweke utaratibu madhubuti unaotekelezeka kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya REA kwa namna inayowezesha ufanisi na tija.

c) Ushirikishwaji mdogo wa viongozi katika maeneo ya Miradi

Kwa kuwa, vijiji na vitongoji vingi katika maeneo ya utekelezaji wa Miradi ya REA awamu ya kwanza na ya pili, kutokana na kutokuwashirikisha viongozi wa maeneo husika,

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha kutokufikiwa kwa malengo ya mradi na kusababisha kero kwa wananchi hasa kwenye maeneo yaliyorukwa,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kuhakikisha kuwa viongozi wa maeneo ambapo miradi ya REA inatekelezwa wanahusishwa ipasavyo, na hasa wakati wa kuainisha vijiji na vitongoji vitakavyohusika.

5.2.2 Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

Mheshimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kuhusu TANESCO, Kamati ina mapendekezo matatu:

a) Wateja wengi kutolipa Ankara za umeme kwa wakati

Kwa kuwa, Taarifa za Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) zinaonesha kuwepo kwa wateja wengi wasiolipa Ankara za umeme inavyostahili na kukwamisha shughuli za Shirika hilo,

Na kwa kuwa, kutokufanyika kwa shughuli za TANESCO kutokana na kuchelewa kupata malipo ya wateja wake, kunazorotesha utendaji na uendeshaji wa TANESCO,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kwamba Bunge, liitake TANESCO kuwachukulia hatuaza kisheria wateja wote wasiolipa Ankara kama inavyostahili.

b) Uharibifu wa Mitambo ya kufua umeme

Kwa kuwa, Mitambo mingi ya kufua umeme imekuwa ikiharibika na kushindwa kufanya kazi kutokana na kutokufanyiwa matengenezo kwa wakati,

Na kwa kuwa, kuharibika kwa mitambo hiyo mara kwa mara husababisha kukosekana kwa umeme wa uhakika nchini jambo linaloigharimu TANESCO na Taifa kwa ujumla,

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri kuwa Bunge liitake Serikali kuliwezesha Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania kumudu kufanya matengenezo ya mitambo ya kufua umeme ili kuliepusha Taifa na tatizo la kukosekana kwa Umeme wa uhakika.

c) Uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme

Kwa kuwa, imebainika kuwa uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme inasababisha kupotea kwa umeme mwingi njiani, jambo linaloathiri kiasi cha umeme kinachowafikia watumiaji,

Na kwa kuwa, upotevu huo unasababisha hasara kwa shirika na upungufu katika ugavi wa meme, hali inayoweza kuathiri uzalishaji na uchumi nchini,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kuiwezesha TANESCO kumudu matengenezo Rekebishi (Rahabilitation) katika vituo na miundombinu ya kusafirishia umeme nchini.

5.2.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Mheshimwa Spika, kuhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kamati ina mapendekezo makuu mawili:

a) Uzalishaji wa Gesi nyingi kuliko inavyonunuliwa

Kwa kuwa, TPDC inao uwezo wa kuzalisha gesi nyingi zaidi ya soko lililopo kwa sasa na kwamba haina uwezo wa kujenga miundombinu ya kusambazia gesi ili kuwafikia watumiaji wengi sokoni,

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha TPDC kuendelea kuwa na gesi isiyonunuliwa na kukosa pesa ambazo ingezipata kwa kuuza gesi ya ziada, jambo linalochangia kuifanya TPDC kushindwa kujiendesha kibiashara kama ilivyo kusudiwa,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuwezesha utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi katika mkoa wa Dar es salaam kwa kuwekeza katika miundombinu ya kusambazia gesi kwa watumiaji.

b) Ufinyu wa bajeti kwa shughuli za TPDC

Kwa kuwa, Taarifa zinaonesha kuwa mapato yote yanayopatikana kwa shughuli za TPDC yanapelekwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali na kwamba bajeti yake hutegemea kiasi kinachotengwa na Serikali,

Na kwa kuwa, uatartabiu huo husababisha TPDC kutengewa bajeti ndogo kuliko kiasi inachopeleka kwenye mfuko mkuu, hali inayokwamisha utekelezaji wa shughuli zake kutokana na ufinyu wa bajeti,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuipatia TPDC bajeti ya kutosha na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya msingi kama inavyotakiwa.

5.2.4 Chuo cha Madini Dodoma (MRI)

Kwa kuwa, Chuo cha Madini Dodoma ndio chuo pekee kinachotoa mafundi mchundo na mafundi sanifu katika sekta ya Madini nchini lakini kinakabiliwa na ufinyu wa bajeti na kuchelewa kupata fedha kwa wakati,

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha chuo kushindwa kudahili wanafunzi wa kutosha kutokana na kushindwa kuajiri walimu wa kutosha pamoja na kujenga miundombinu ya mafunzo, jambo linaloongeza upungufu wa mafundi mchundo na mafundi sanifu wanaohitajika,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kukiwezesha chuo hiki kifedha kwa kukitengea bajeti ya kutosha.

5.2.5 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)

Kwa kuwa, Wakala wa Jiolojia nchini amepewa jukumu muhimu la kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza taarifa mbalimbali za kijiosayansi, kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya ardhi (Earth),

Na kwa kuwa, kutokuwezesha kibajeti kwa TAASISI hiyokunachangia utekelezaji hafifu wa majukumu hayo muhimu na kusababisha Taifa kukosa taarifa za msingi kuhusiana na jiolojia ya nchi,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri serikali kuwezesha Wakala wa Jiolojia nchini kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ikiwemo kufanya tafiti mbalimbali kuhusu majanga kama vile, matetemeko ya Ardhi, Milipuko ya Volcano na maporomoko ya ardhi, kwa lengo la kuiliwezesha Taifa kukabiliana na majanga hayo.

5.2.6 Sekta Ndogo ya Mafuta

Mheshimwa Spika, kwenye Sekta ya Mafuta nchini, Kamati ina mapendekezo makuu mawili:

a) Umuhimu wa Matenki ya Kuhifadhia Mafuta

Kwa kuwa, matenki ya kuhifadhia mafuta (Farm Tanks) ni muhimu kwa ajili ya kuiwezesha serikali kudhitbiti hujuma za Wafanya biashara ya mafuta nchini pamoja na kuinongezea Serikali mapato,

Na kwa kuwa, kukosekana kwa Metnki hayo kunasabaisha hatari ya kushindwa kudhibiti itakapotokea hujuma za makampuni ya mafuta nchini hali ambayo awali ilikuwa ikidhibitiwa na TPDC,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuiwezesha TPDC kuwekeza katika Ujenzi wa matenki hayo.

b) Bei elekezi kutokuzingatia umbali kutoka makao makuu ya miji/wilaya

Kwa kuwa, uuzaji wa mafuta nchini huongozwa na bei elekezi ambayo kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati, haizingatii tofauti iliyopo ya umbali kutoka makao makuu ya miji/ wilaya,

Na kwa kuwa, Kutokuzingatiwa kwa tofauti hiyo ya umbali kunasababisha wauzaji wa mafuta kuuza kwa bei ambayo inawaumiza wananchi, jamba linalohitaji kuwekewa utaratibu bora,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuhakikisha kuwa bei zote elekezi za mafuta zinazingatia umbali uliopo kutoka makao makuu ya miji/wilaya.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Ndugai Spika, Dr. Tulia Akson Naibu Spikana Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Mohamed Juma Khatibu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Susan limbweni Kiwanga, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Maulid Said Abdallah Mtulia, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Desderius John Mipata, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb	Mjumbe
24. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb	Mjumbe
25. Mhe. John Wegesa Heche, Mb	Mjumbe

Pia Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati na Madini chini ya uongozi wa Mhe. Prof. Sospeter Muhongo(Mb) Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake Dr. Medard Matogolo Kalemani na watendaji wote wa wizara kwa ushirikiano walioutoa katika

kipindi hiki ambao umeiwezesha Kamati yako kutekeleza majukumu yake kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushirikiano wake na Kamati yetu. Pia namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Doto Mashaka Biteko, Mb
Mwenyekiti
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini
Januari, 2017